UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA

Oktoba 18, 2019

# Sintofahamu watumishi wa umma kujiandikisha uchaguzi serikali za mitaa

**Waandishi Wetu**, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Dar/mikoani.** Wakati shughuli ya kuandikisha wapigakura wa uchaguzi wa serikali za mitaa zikifungwa jana, kitendo cha baadhi ya watendaji wakuu wa taasisi za Serikali kuonyesha lugha inayoonekana kushinikiza wafanyakazi kujiandikisha imeibua sintofahamu.

Barua za baadhi ya viongozi wa manispaa na vyuo vikuu zilizosambaa katika mitandao ya kijamii zinaonyesha kuwataka watumishi kuhakikisha wanajiandikisha, jambo ambalo baadhi ya wachambuzi waliozungumza na *Mwananchi* wamesema si sahihi.

Na kusambaa kwa barua hizo kumemfanya Waziri wa Tamisemi, Seleman Jafo kutoa ufafanuzi.

Jafo alikaririwa juzi akizungumzia barua ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma iliyotoa maelekezo kwa watumishi kujiandikisha. "Niliongea na mkurugenzi (wa Dodoma) kujua kuna kitu gani kiliendelea na yeye akaniambia lengo lao kubwa ilikuwa ni kuhamasisha watumishi kwa sababu wao wanafanya kazi mamlaka za serikali za mitaa," alisema.

Dodoma iliwaandikia barua wakuu wa idara na vitengo, watendaji wa kata na waratibu wa elimu ili kuwatambua watumishi wa umma waliojiandikisha.

Pia kulisambaa taarifa ya kuwataka watumishi wa halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kujiandikisha kupiga kura, lakini haikuwa na majina.

Pia, Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) kimewataka wakuu wake wa vitengo kuwatambua watumishi wa umma waliojiandikisha, huku ikieleza uwasilishaji huo wa majina utakavyokuwa.

Barua ya chuo hicho iliyosambaa mitandaoni inaeleza kuwa taarifa za watumishi waliojiandikisha zilitakiwa kabla ya juzi na kupelekwa ofisi ya naibu makamu mkuu wa chuo hicho.

"Kwani sisi watumishi ndio tumesababisha mwamko huo mdogo? Watafute kiini sio waanze kutaka kutokea kwa watumishi wa umma. Hata sisi tuna haki zetu kama raia," alisema mmoja wa watumishi aliyezungumza na *Mwananchi* kwa sharti la kutotajwa jina.

Katika maelezo yake ya juzi, Waziri Jafo alisema: "Kuna video inasambaa kuwa ambao hawajajiandikisha wanyimwe huduma za kijamii. Suala la kujiandikisha na kupiga kura ni la hiari isipokuwa tunahamasishana watu waende kupiga kura."

**DONDOO**

**Waziri wa Tamisemi, Seleman Jafo alikaririwa akisema hadi Oktoba 14, mwaka huu walikuwa wamejiandikisha watu milioni 15 na kwamba matarajio ni watu milioni 22**



Alisema kutaka wasiojiandikisha wanyimwe huduma za kijamii katika mitaa, vitongoji na vijiji wanavyoishi si maelekezo ya Tamisemi isipokuwa watu wahamasishane.

"Kujiandikisha ni jambo la msingi kwa sababu tutakuwa tunatambuana katika maeneo yetu. Sijui eti mtu atapelekwa katika chombo cha sheria no (hapana)," alisisitiza.

Kuhusu barua ya mkurugenzi wa Jiji la Dodoma kuagiza watumishi wote wa umma waliojiandikisha watambuliwe, alisema suala hilo inaonekana maandishi hayakuwa sawa.

"Ilikuwa ni kuona watumishi wa mamlaka husika wao wawe kipaumbele. Lengo kubwa si kuwafanya watu kwamba mwisho wa siku watawajibishwa au kufukuzwa, hapana," alisema.

"Kama ilikuwa ni hamasa basi maandishi hayakuwa vizuri. Inawezekana tafsiri haikuwa hivyo, lakini jambo lililokuwepo na jinsi gani watumishi waweze kujiandikisha ili kuchagua viongozi wao," alisema Jafo.

Kwa nyakati tofauti *Mwananchi* ilimtafuta msemaji wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (Talgwu) aliyesema yupo katika kikao huku rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (Tucta), Tumaini Nyamhokya akitaka kufuatwa ofisini ili kutoa ufafanuzi wa jambo hilo.

## Maoni ya wachambuzi

Dk Richard Mbunda wa Chuo Kikuu Dar es Salaam (Udsm) alisema utaratibu mpya unaotumika sasa wa kuwaandikisha watumishi wa umma nchini, umewashtua. "Hili jambo limetushtua hasa sisi wachambuzi wa siasa kwa sababu kujiandikisha na kupiga kura linatakiwa liwe suala la hiyari. Katika mfumo wa kidemokrasia hatulazimishani," alisema.

"Inatakiwa watu waelimishwe ili waende kujiandikisha na baadaye kupiga kura kwa sababu kutojiandikisha watu huwa wanatuma meseji kwa namna nyingi. Inatakiwa watu wenyewe waone kwamba wana wajibu wa kufanya hivyo na wafanye. Sio kwa kulazimishwa.

"Kama ambavyo sasa watumishi wanatishiwa. Hapana. Huko ni kutafuta uhalali kwa nguvu. Ukimlazimisha mtu akapige kura akampigie nani? Ukiwalazimisha wanaweza kuharibu kura."

Naye wakili wa Mahakama Kuu, Frank Mushi alisema haki ya kupiga kura haizalishi kosa la jinai iwapo mtu ataamua asiitumie na hakuna sheria inayomlazimisha ajiandikishe.

"Ndio maana umeshasikia miaka yote wapigakura waliojitokeza ni wachache lakini hujawahi kusikia msako wa wasiopiga kura ili wafikishwe mahakamani. Ni suala la hiyari," alisema.

Mbunge wa Kigoma Mjini (ACT-Wazalendo), Zitto Kabwe alisema hakuna sheria inayoweza kumbana mtumishi ikiwa hajajiandikisha, "kwa hiyo utafanya nini kwa ambao hawatasajili? Utawatoa kazini? Kuwaadhibu au chini ya sheria gani? Wasiwasi wangu ni unyanyasaji kwa watumishi wa umma ambao hawataki kutumia haki yao ya kupiga kura."

## Siku ya mwisho uandikishaji

Katika maeneo ya Dar es Salaam idadi ya waliojitokeza kujiandikisha ilionekana kuwa ndogo huku sababu kadhaa zikitajwa, baadhi ya mawakala kueleza kuwa wamekuwa wakizuiwa kuwahoji wanaokwenda kujiandikisha.

"Tukauliza kwa nini tuzuiliwe kuuliza wakati ndiyo kazi yetu hapa kituoni? Hatukujibiwa ila tuliambiwa hicho ndiyo tunatakiwa kuzingatia," alisema Lucy Mange, wakala wa Chadema kituo cha Ofisi za Serikali ya Mtaa wa Mabibo.

Wakala wa CCM kituoni hapo Sikujua Ngonyani aliunga mkono madai hayo akifafanua licha ya zuio hilo waliamua kutumia nguvu kuendelea kuhoji wakiamini nafasi yao imefanikisha kuwatambua wengi wasiokuwa na sifa ya kujiandikisha mtaani hapo.

Mawakala Bahati Shani na Maua Athani (ACT-Wazalendo), Triphon Makata(CCM), Stella Julia (CUF) na Augustine Kashuli (Chadema) wa vituo viwili vilivyopo Serikali ya Mtaa wa Sokoni walisema mwitikio ni mdogo kwa sababu kadhaa ikiwamo kukatishwa tamaa na viongozi wanaomaliza muda wao.

Mkoani Mara, hadi Oktoba 16, 2019, zaidi ya watu 631, 568 walikuwa wameandikishwa kwa ajili ya kupiga kura katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24.

Akizungumza na *Mwananchi* jana, katibu tawala mkoa wa Mara, Karolina Mthapula alisema walioandikishwa ni wanaume 303, 951 na wanawake 327, 617, sawa na asilimia 63.7 ya lengo la kuandikisha watu 991, 388.

**KWA TAARIFA YAKO**

**Neno refu zaidi la Kiingereza lina herufi 189,819.**